Mtazamo Yetu Dhidi Ya Mungu Sehemu Ya 1 – Je Unamstahi, Unampenda, Unamuamini, Na Kumshukuru?

(Attitude Towards God Part 1- Do You Reverence, Love, Trust, And Thank Him?)

Na

Ellis P. Forsman

Mtazamo Yetu Dhidi Ya Mungu Sehemu Ya 1 – Je Unamstahi, Unampenda, Unamuamini, Na Kumshukuru?

Na

Ellis P. Forsman

Octoba 6, 2011

Mtazamo Yetu Dhidi Ya Mungu Sehemu Ya 1 – Je Unamstahi, Unampenda, Unamtegemea, Na Kumshukuru?

Mithali 23:7

Mtazamo njema kimsingi ni muhimu.

Zaburi 100:2-4, "*Mtumikieni BWANA kwa furaha, njooni mbele zake kwa kuimba; jueni kwamba BWANA ndiye Mungu; ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake; tu watu wake na kondoo wa malisho yake. Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; nyuani mwake kwa kusifu; mshukuruni, lihimidini jina lake;*"

Tabia njema ni muhimu kwa umoja katika kanisa la sehemu fulani. Karama zote zilizopo duniani haziwezi kuunda nia mbaya ambayo tunaweza kuwa nayo. Mith. 23:7, "*Maana aonavyo nafsini mwake ndivyo alivyo…*"

Kwa nia njema, juhudi zetu za kumtumikia Bwana hurithiwa na kuwa katika hali timilifu.

Tabia hutafsiriwa: Ni hali ya akili au hisia, kutokuwa katika nafasi.

Kwa maneno mengine, ni kusudi la mtu juu ya kitu fulani.

Kidini tunaweza kuwa na tabia iletayo baraka kutoka kwa Mungu, au ile isiyo leta rehema kutoka kwake. Tunapaswa kuwa na tabia njema katika maisha haya kama tunatarajia kupokea baraka zake.

Ebu tuangalie baadhi ya tabia tunazopaswa kuwa nazo dhidi ya Mungu.

Tunapaswa Kuwa Na Tabia Ya Kuheshimu

Hapo mwanzo niliwahi kusikia mtu anaomba maombi yafuatayo: "Wewe, Baba Mkubwa. Wewe ni mwanadamu! Mambo yanaendaje huko juu mbinguni…"

Ni tabia isiyo na adabu kiasi gani.

Kumtumikia Bwana huanza na tabia ya nidhamu.

Mith. 1:7, "*Kumcha BWANA ni chanzo cha maarifa, bali wapumbavu hudharau hekima na adabu.*

Kumtumikia Bwana huanza na adabu ya nidhamu kwa sababu ya Yeye alivyo.

- Zaburi 89:5-11, "*Ee BWANA, mbingu zitayasifu maajabu yako, uaminifu wako katika kusanyiko la watakatifu. Maana ni nani katika mbingu awezaye kulinganishwa na BWANA? Ni nani afananaye na BWANA miongoni mwa malaika? Mungu huogopwa sana barazani pa watakatifu, ni wa* ***kuhofiwa*** *kuliko wote wanaomzunguka. BWANA, Mungu wa majeshi ni nani aliye hodari kama wewe, Ee YAHU? Na uaminifu wako unakuzunguka. Wewe ndiye ukitawalaye kiburi cha bahari. Mawimbi yake yainukapo wayatuliza wewe. Ndiwe uliyemseta Rahabu akawa kama aliyeuawa, kwa mkono hodari umewatawanya wakuchukiao. Mbingu ni mali yako, nchi nayo ni mali yako, ulimwengu na vyote viujazavyo ndiwe uliyeupiga msingi wake.*" Kuhofiwa katika kifungu hiki – 3372 yahu' – (Heb) kuogopa, kuhofu; kuhofia.

- Mat. 21:33-39, "*Sikilizeni mfano mwingine, kulikuwa na mtu mwenye nyumba, naye alipanda shamba la mizabibu akalizungusha ugo, akachimba shimo la shinikizo, akajenga mnara, akapangisha wakulima akasafiri. Wakati wa matunda ulipokuwa karibu, akawatuma watumwa wake kwa wale wakulima, wapokee matunda yake. Wale wakulima wakawamata watumwa wake, huyu wakampiga, na huyu wakamwua, na huyu wakampiga kwa mawe. Akawatuma tena watumwa wengine wengi kuliko wa kwanza wakawatenda vile vile. Mwishowe akamtuma mwanawe kwao, akisema* ***watamstahi*** *mwanangu. Lakini wale wakulima walipomwona yule mwana wakasemezana wao kwa wao, huyu ni mrithi; haya na tumwue, tuutwae urithi wake. Wakamkamata wakamtupa nje ya shamba la mizabibu, wakamwua.*" Kustahi katika kifungu hiki – 1788 entrepo {en-trep'-o} (Kiyunani.) (1) kumuabisha mtu (2) kuaibishwa (3) kumsitahi mtu (4) kugeuka (KJV: kustahi 4, kujali 2, kuabishwa 2, aibu 1).

- Heb. 12:28-29, "*Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemeshwa, na mwe na neema ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na **unyenyekevu** na kicho; maana Mungu wetu ni moto ulao.*" Hii ni aidos 0127 {ahee-doce'} (Kiyunani.) (kupitia wazo la mtazamo wa chini) (1) hali ya aibu au heshima, nadhifu, hofu, unyenyekevu, kujali kwa wengine, heshima (KJV: kuwa na aibu usoni 1, kustahi 1). Ina maana inayofanana na aibu ya uso kama hii ya kifungu kifuatacho: 1 Tim. 2:9, *"Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya **kujisitiri**, pamoja na adabu nzuri na moyo..."*

Tunapaswa kumwonyesha Mungu heshima tunapoomba; tunatakiwa kufanya hivyo kwa njia ya unyenyekevu.

Zaburi 95:2-7, "*Tuje mbele zake kwa shukrani; tumfanyie shangwe kwa zaburi. Kwa kuwa BWANA ni Mungu mkuu, na mfalme mkuu juu ya miungu yote. Mikononi mwake zimo bonde za dunia, hata vilele vya milima ni vyake. Bahari ni yake, ndiye aliyeifanya, na mikono yake iliumba nchi kavu. Njooni, tuabudu, tusujudu, **tupige magoti** mbele za BWANA aliyetuumba. Kwa maana ndiye Mungu wetu, na sisi tu watu wa malisho yake, na kondoo za mkono wake. Ingekuwa heri leo msikie sauti yake!*" Maana hapa ni mara 3766 kara (Kiebrania.) kukunja goti; kuzama, kusujudu.

Hata wakati tunapoimba nyimbo za sifa kwake na tunafurahi kwa tendo hilo, tunapozungumza na Mungu katika kuomba tunapaswa kunyenyekea mbele zake kwa sababu ya yeye jinsi alivyo.

Rum. 14: 11, "*Kwa kuwa imeandikwa, kama niishivyo, anena Bwana, kila goti litapigwa mbele zangu; na kila ulimi utamkiri Mungu.*"

Paulo akiwaaga Waefeso, alikuwa na mashaka kuhusu kuanguka kwao kutoka kwa Mungu na akawafundisha kwa majonzi kwa miaka mitatu. Aliwaita pamoja kwa wakati mmoja wa mwisho kwa maana alijua ataenda kufungwa Rumi. Alipomaliza kuwahutubia, angalia tabia ya Paulo dhidi ya Mungu alipoomba. Mdo. 20:36, "*Alipokwisha kunena haya, akapiga magoti, akaomba pamoja nao wote.*"

Kwa kupiga kwake magoti katika maombi, alikuwa ananyenyekea mwenyewe mbele za Mungu.

Yak. 4:10, "***Jidhilini*** *mbele za Bwana, naye atawakuza.*" Jidhili inamaana ifuatayo: 5013 tapeinoo {tap-i-no'-o} (Kiyunani.) (1) kufanya iwe chini, kuleta chini (1a) kulinganisha, punguza katika usawa (1b) kiunganishi. Kuleta katika hali ya unyenyekevu, kupunguza katika hali ya kumaanisha (1.b.1) kuweka katika hatua ya chini au kwa sehemu (1.b.2) kupungua (1.b.3) kuwekwa katika kiwango cha wengine wanao heshimiwa au tuzwa (1.b.4) kunyenyekea au kushuka mimi mwenyewe kwa maisha ya unyenyekevu (1.c) kupungua, kukandamizwa (1.c.1) ya nafsi ya mtu kuleta kiburi chini (1.c.2) kuwa na wazo la kujidhili ya mtu binafsi (1.c.3) kuwa na adabu katika hali isiyo fikirika (1.c.4) kuachana na kila aina ya ubaya (KJV: nyenyekea 6, shuka 5, nyenyekea (mtu) binafsi 2, kuleta chini 1).

Mfano: Luka 18:10-14, "*Watu wawili walipanda kwenda hekaluni kusali, mmoja Farisayo, wa pili mtoza ushuru. Yule Farisayo akasimama akiomba hivi moyoni mwake; Ee Mungu nakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine, wanyang'anyi, wadhalimu, wazinzi, wala kama huyu mtoza ushuru. Mimi nafunga mara mbili kwa juma; hutoa zaka katika mapato yangu yote. Lakini yule mtoza ushuru alisimama mbali, wala hakudhubutu kuinua macho yake mbinguni, bali alijipigapiga kifua akisema Ee Mungu uniwe radhi mimi mwenye dhambi. Nawaambia huyu alishuka kwenda nyumbani kwake amehesabiwa haki kuliko yule; kwa maana kila ajikwezaye atadhiliwa, naye* ***ajidhiliye*** *atakweza.*"

Angalia katika shauri hili kwamba wote Mfarisayo na mtoza ushuru walisimama walipokuwa wanaomba. Lakini mtoza ushuru alinyenyekea sana kuliko Mfarisayo. Ni kwa sababu alijishusha mwenyewe katika roho yake; tabia yake ilikuwa tofauti.

Je hii inamanisha kwamba tunapaswa kupiga magoti kila mara tunapoomba? Angalia kifungu kifuatacho: Marko 11:25, "*Nanyi kila msimamapo na kusali, sameheni mkiwa na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu.*"

Tunaweza kupata mifano kutoka katika Biblia wanadamu wakisali wakiwa wamesimama, kuinamisha vichwa, kupiga magoti, hata katika nyuso zao. Kilichomuhimu ni kwamba tunaposali, kwamba tunafanya hivyo katika hali ya kunyenyekea. Yakobo 4:6, "*Lakini hutujalia sisi neema iliyozidi; kwa hiyo husema Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema wanyenyekevu.*

Kumtumikia Bwana huanza na tabia ya heshima kwa sababu ya jinsi tulivyo.

Mungu alituumba na tuliumba ili kumtumikia. Zaburi 100:2-4, "*Mtumikieni BWANA kwa furaha; njooni mbele zake kwa kuimba; jueni kwamba BWANA ndiye Mungu; ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake, tu watu wake na kondoo wa malisho yake. Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; nyuani mwake kwa kusifu; mshukuruni, lihimidini jina lake:*"

Watu wengine wanatabia kwamba hawamuhitaji Mungu; kwamba wanaweza kujijali wenyewe.

Napoleon alikuwa na tabia kama hizi. Alipanga kuvamia Urusi na kumshinda Czar. Mtu mmoja akasema mbele yake, "Mwanadamu hupendekeza, lakini Mungu hamiliki." Kwa kusikia kauli hii, Napoleon akajibu, "Ninapendekeza na similiki." Kwa maksudi kabisa aliamuacha Mungu katika mfumo mzima, na ikadhihirisha kufisha. Kwa maana Mungu alimshughulikia Napoleon kupitia moja ya kiumbe chake kidogo na kuvunjika – mruka kwenye barafu. Jeshi lake halikujianda kwa ajili ya barafu ya Urusi, na alishindwa. "Urusi itakuwa yangu," moyo wake wenye kiburi ulisema, lakini Mungu alikuwa pale.

Kwa nini wote tunamhitaji Mungu? Ni kwa sababu wote tumetenda dhambi. Rum.3:23, "*Kwa sababu wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.*"

Hakuna hata mmoja wetu anayeweza kuzishughulikia dhambi zetu wenyewe. Wote tunahitaji msaada wa Mungu ili kuzifuta dhambi zetu. Mdo. 8:18-24, "*Hata Simoni alipoona ya kuwa watu wanapewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya mitume, akataka kuwapa fedha akisema, nipeni na mimi uwezo huu, ili kila mtu nitakayemwekea mikono yangu, apokee Roho Mtakatifu. Lakini Petro akamwambia fedha yako na ipotelee mbali pamoja nawe, kwa kuwa umedhania karama ya Mungu yapatikana kwa mali. Huna fungu wala huna sehemu katika jambo hili, kwa kuwa moyo wako si mnyofu mbele za Mungu. Basi tubia uovu wako huu, ukamwombe Bwana ili yamkini usamehewe fikira hii ya moyo wako. Kwa maana nakuona u katika uchungu kama nyongo, na tena u katika kifungo cha uovu. Simoni akajibu akasema, Niombeeni ninyi kwa Bwana, yasinifikilie mambo haya mliyosema hata moja.*"

Tunaweza kumuomba Mungu sisi wenyewe; tunaweza kuwaomba wengine waombe kwa niaba yetu; lakini ni Mungu pekee anayeweza kutusameehe dhambi zetu pale ambapo mahitaji yetu hutekelezwa. Tunapomwacha Mungu nje ya maisha yetu, tunabaki kuwa katika hali ya dhambi. Hatuwezi kuishi katika tabia ~~ya "Naweza kuishi bila Mungu" au "Simhitaji Mungu."~~

Kumtumikia Bwana huanza na tabia ya nidhamu kwa sababu ya kile alichotufanyia.

Zaburi 111:9, "*Amewapelekea watu wake ukombozi, ameamuru agano lake liwe la milele, jina lake ni takatifu la* ***kuogopwa***."

Ni Mungu tu ndiye aliyekirimiwa jina hili. Anapaswa kuheshimiwa.

- Efe. 1:3-7, "*Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu war oho ndani yake Kristo; kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo. Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ilitufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na Uradhi wa mapenzi yake. Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika katika huyo mpendwa. Katika yeye huyo, katika damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake.*"

- Tito 2:14, "*Ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema.*"

Kwa sababu ni mtakatifu na alizikomboa dhambi zetu kwa damu ya Yesu msalabani, tunapaswa kuwa na tabia ya heshima kwake kwa njia na mfumo tunaoishi; tunapaswa pia kuwa watakatifu (takaswa) kwa sababu ametukomboa kutoka katika maovu ya dunia. Tunapaswa kuwa tofauti kuliko dunia (wateule), na tuwe na tabia ya shauku katika matendo mema ya Kikristo.

Hebu wote tuwe na tabia njema nya nidhamu ya Mungu katika maisha yetu.

Tunahitaji Tabia Ya Upendo

Tunapaswa kuwa na upendo mwema dhidi ya Mungu – inapaswa kuwa ya kweli.

Na upendo wetu lazima uwe jumla. Mat. 22:37, "*Akamwambia, mpende Bwana Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote.*"

Tunaonyesha upendo wetu kwake tunapomjumuisha katika Nyanja zote za maisha yetu; tunamjumuisha katika maamuzi yetu tunayopaswa kufanya. Tukishindwa, upendo wetu haujakamilika.

Upendo wetu lazima uwe wa utii.

- Yohana 14:15, "*Mkinipenda, mtazishika amri.*"
- Yohana 14:24, "*Mtu asiyenipenda, yeye hazishiki maneno yangu, nalo neno mnalolisikia sio langu, ila ni lake Baba aliyenipeleka.*"

Tunapolitii neno lake tunamuonyesha hakika kwamba tunampenda. Tuwe na tabia ya upendo wa utii katika maisha yetu, kama Daudi alivyofanya.

Zaburi 119:97, "*Sheria yako naipenda mno ajabu, ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa.*"

Upendo wetu unapaswa kuigwa.

Mat. 22:38-39, "*Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo,nayo ni hii, mpende jirani yako kama nafsi yako.*"

Kama upendo wetu kwake ukikamilika, itaonyeshwa katika maisha yetu kwa wale wanaotuzunguka.

Upendo unafaa kuwa msukumo wa kila kitu tunachokifanya.

1 Kor. 13:1-3, "*Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote, na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo si kitu mimi. Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo hainifaidii kitu.*"

Tunaweza kuwa na ujuzi wote wa Biblia tunaoweza kuhubiri neno la Mungu kwa mamilioni ya watu duniani kote, lakini kama hatuna upendo miyoni mwetu kwa wale watuzungukao, yote ni kwa sifuri. Yohana 13:35, "*Hivyo watu wote watatumbua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.*"

Ni Lazima Tuwe Na Tabia Ya Imani Na Tumaini

Imani ni msukumo wenye nguvu na tumaini katika mambo yasiyoonekana. Heb. 11:1, "*Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.*"

Pasipo imani, haiwezekani kumpendeza Mungu.

Heb. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*"

Imani inayozungumzwa kwenye Waebrania 11 walikuwa WATENDAJI . . .Imani yao ILIFANYA KAZI!

Ndugu na dada, wasioamini, wasio na imani, na wasiotii vyote nit oleo la neno la Kiyunani linalofanana.

Wasioamini – 0570 apistia {ap-is-tee'ah}(Kiyunani.) (1) Wasio na imani, asiyeamini (2) itaji la imani, kutoamini (3) imani ovu.

Kutotii – 0543 apeitheia {ap-i'-thi-ah}(1) kuacha, kukaidi matakwa mema (KJV: kutoamini 4, kutotii 3).

Hitimisho la mara zote, tunapaswa kufanya ni kwamba kuamini, imani na utii zote zinahusiana na kila mmoja, na huweza kutumiwa kwa kubadilishana.

Baadhi katika ulimwengu wa dini wana wazo kwamba kitabu cha Yakobo haipo katika Biblia kwa sababu inasema kwamba imani pasipo matendo imekufa. Utii ufanana na neno imani. Mifano yote ya imani katika sura ya 11 ya Waebrania ilijumuisha matendo.

- Heb. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*"
- Rum. 10:13-21, "*Kwa kuwa kila atakayeliita jina la Bwana ataokoka. Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikiaje pasipo mhubiri? Tena wahubirije wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, ni mizuri kama nini miguu yao wahubiriyo habari ya mema! Lakini si wote walioitii ile habari njema. Kwa maana Isaya asema, Bwana, ni nani aliyeziamini habari zetu?* ***Basi imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa neno la Kristo***. *Lakini nasema wao hawakusikia?*

Naam, wamesikia, sauti yao imeenea duniani mwote, na maneno yao hata miisho ya ulimwengu. Lakini nasema je Waisraeli hawakufahamu? Kwanza Musa anena, nitawatia wivu kwa watu ambao si taifa, kwa taifa lisilo na fahamu, nitawaghadhibisha. Na Isaya anao ujasiri mwingi asema, nalipatikana nao wasionitafuta, nalidhihirika kwao wasioniuliza. Lakini kwa Israeli asema, mchana kutwa naliwanyooshea mikono watu <u>wasiotii</u> *na wakaidi.*"

- "*Mchana kutwa naliwanyooshea mikono watu <u>wasio na imani</u> na wakaidi.*"
- "*Mchana kutwa naliwanyooshwa mikono watu <u>wasioamini</u>.*"
- "*Mchana kutwa naliwanyooshea mikono watu <u>wasiotii</u> na wakaidi.*"

Imani inaweza kubadili utambuzi wetu dhidi ya Mungu na jinsi tunavyozichukulia amri zake.

Imani na taraja hututia nguvu kushinda wasiwasi.

Mat. 6:30, "*Basi ikiwa Mungu huwavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo na kesho hutupwa hutupwa kalibuni, je hatazidi sana kuwavika ninyi enyi wa imani haba?*"

Wakati mwingine tunakuwa na wasiwasi juu ya vitu na hali iliyopo katika maisha haya, tukienda tuki hofu, na kujaribu kujali vitu kivyetu. Tunaweza kujikuta wenyewe katika hali ya uhitaji wa pesa; hivyo tunachukuwa kazi nyingine. Tatizo ni kwamba tumeondoa imani na tumaini letu kwa Mungu ambaye ameahidi kwamba ajashughulikia matatizo yetu. Tunafanya kila tuwezalo, hatupaswi kuwa na wasiwasi na kuhofia vitu kama hivyo.

Imani na tumaini hutupa nguvu kushinda kukata tama.

Msikilize mtume Paulo aliyevumilia mengi, bado hakuwa na wasiwasi. 2 Kor. 4:7-17, "*Lakini tunahazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu. Pande zote twadhikika, bali hatusongwi, twaona shaka bali hatukati tama. Twaudhiwa bali hatuachwi; twatupwa chini bali hatuangamizwi; siku zote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhiirishwe katika miili yetu. Kwa maana sisi tulio hai, siku zote twatolewa tufe kwa ajili ya Yesu, ili uzima wa Yesu udhiirishwe katika miili yetu ipatikanayo na mauti.*

Basi hapo mauti hufanya kazi ndani yetu, bali uzima ndani yenu. Lakini kwa kuwa tuna roho ile ile ya imani, kama ilivyoandikwa naliamini, na kwa sababu hiyo nalinena; sisi nasi twaamini na kwa sababu hiyo twanena; tukijua ya kuwa yeye aliyemfufua Bwana Yesu atatufufua sisi nasi pamoja na Yesu, na kutuhudhurisha pamoja nanyi. Kwa maana mambo yote ni kwa ajili yenu ili neema hiyo ikiongezwa sana, kwa hao walio wengi shukrani izidishwe, na Mungu atukuzwe. Kwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wan je unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku. Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele, uzidio kuwa mwingi sana."

Kama naweza kufa nikiwa namfanyia Bwana kazi, namuomba Mungu niwe na imani kama hiyo na kuamini katika Bwana kunibeba. Tunapaswa wote kuwa na aina hiyo ya tabia ambayo Paulo alikuwa nayo.

Imani na tumaini hututia nguvu kuishinda dunia.

1 Yohana 5:4, "*Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu, na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu.*"

Tabia Ya Kushukuru

Maneno ni muhimu sana. Yanatusaidia au kutuvunja. Wakati fulani nilisikia, na nikaiamini, kwamba maneno matatu ya Kiingereza ni: nakupenda." Vilevile maneno mawili matamu yanayosemwa ni, "Asante."

"Asante!" Kuna kitu cha kipekee kuhusu maneno haya:

Miaka ya hivi karibuni imekuwa ikiitwa "uonyesho uliopotea." Imepotea kwa sababu hutumika mara chache sikuizi.

Kwa baadhi ya sababu – bila shaka moja ni ubinafsi – watu wameacha maneno haya mazuri. Kila Mkristo anapaswa kuwa na tabia hii ya shukrani, hasa kwa Mungu. Kol. 3:17, "*Na kila mfanyalo kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.*"

Sio vigumu kuwa mtu mwenye shukrani tunapohesabu baraka zetu nyingi. Zaburi 126:3, "*BWANA alitutendea mambo makuu, tulikuwa tukifurahi.*"

Tabia ya shukrani kwa baraka tulizonazo:

- Utasaidia kuondoa uchungu na utengano katika maisha yetu.
- Utasaidia kusimika maudhurio ya wazi, ibada ya kweli, maisha matakatifu, huruma, na upendo katika maisha yetu.

Ghadhabu ya Mungu imefunuliwa dhidi ya wanadamu kwa sababu nyingi, lakini maandiko yanasema itakuwa pia kwa wale wasio kuwa na shukrani.

Rum. 1:18-21, "*Kwa maana ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni juu ya uasi wote na uovu wa wanadamu waipingao kweli kwa uovu. Kwa kuwa mambo ya Mungu yanayojulikana yamekuwa dhahiri ndani yao, kwa maana Mungu aliwadhihirishia. Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake, yaani, uweza wake wa Uungu wake; hata wasiwe na udhuru. Kwa sababu walipomjua Mungu hawakumtukuza kama ndiye Mungu <u>wala kumshukuru</u>; bali walipotea katika uzushi wao na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza.*"

Hitimisho

Je tabia yako dhidi ya Mungu ndivyo inavyopaswa kuwa?

- Unajidhili
- Penda
- Imani na tumaini
- Tunakusudia

Tabia zetu!! Chaguo ni letu!! 1 Sam. 12:24, "*Mcheni BWANA tu, mkamtumikie kwa mioyo yenu yote, maana kumbukeni jinsi alivyowatendea mambo makuu.*"